KISWAHILI MARKING SCHEME

1. SHAIRI(LAZIMA)

(a) mwerevu hajinyoi 1 x1- alama 1

(b) toni ya mashairi ni ya masuto na maonyo 2 x 1 = alama 2

(c) Dhamira ya shairi ni kukashifu/kusuta walionavyo wasiothamini wengine wenzao 2 x1 = ala 2

(d) una mishororo minne
-Una vipande 2 (ukwapi na utao)=katika kila mshororo
-Kila mshororo una mizani 16(8,8).

| | | |
|---|---|---|
| Vina | na | vu |
| | na | vu |
| | na | vu |
| | vu | we |

4 x 1 = alama 4

e) Jazada – 'kisu gutu' 1 x2= alama 2

f) inkisari- Km 'meonekana,megeuka'nk

Lahaja – Km. Ndiya-jia
Maivu-yalbiva

Mazda KM. mwerevu
Tabidila. Km – ujuwe,waliyo,akajinyowa mwerevu 3 x 1 = alama 3

g) -Kutajilika kusipumbaze ukafikiri kuwa una maarifa sana. Kuringa kwako ndiko kutakuangamiza

-Wakati utafika ambapo utapatwo na hali ngumu usioweza kujinasua
-Hata mtu awe na maarifa au uwezo hajitoshelezi kwa kila kitu.
(alama 4)

h) (i) Kitu – mali au utajiri
(ii) Mtovu – maskini
2 x 1 – alama 2

2 (a)

- Maneno haya ni ya Balozi wa Mtemi Nasaba Bora.
- Walikuwa uwanjani wa Nasaba Bora.
- Anamsifu Mtemi kwa kusema kuwa ana utambuzi kuliko wazungu.
- Walikuwa wakisherehekea sikukuu ya Wazalendo.

Alama 4

(b) Kinyume cha kauli hii.
- Nasaba Bora alipokuwa katika Wizara ya Ardhi na makao, anaficha faili za raia badala ya kuwatolea huduma.
- Utawala wa Uingereza na ule wa Tornoko huru unazisaliti juhudi za mashujaa kwa kutowafidia mashujaa k.v. Matuko Weye.

- Viongozi wa Sokomoko wanausaliti wajibu wao kuboresha uongozi. Wanamsifu Nasaba Bora, kiongozi badala ya kumkosoa k.v Balozi.
- Mashamba aliyoiba alijitengenezea faili ili zimfae.
- Serikali inamtelekeza Chechwe, baada ya kuumia akichezea timu ya taifa.

Zozote 5 x 2 = alama 10

(c ) Sifa za mzungumzaji – Balozi

- Mbinafsi.
- Mpyoro – maneno makali.
- Mwenye tamaa.
- Ni barakala ( mpenda cheo)
.
- Ni mwongo / mdanganyifu.
- Ni katili. Zozote 6 x 1 = alama 6

Q3 (i) wanaendeleza wizi wa mali ya umma hivyo kudidimiza maendeleo. Mf. Nasaba Bora anaiba/nyakua mali ya Chichiri Hamadi na Mwinyihatibu Mtembezi

(ii) Wanahusika katika mauaji ya raia. Mf Nasaba Bora anatuma watu kumuua Chichiri. Pia anawatuma askari kumpiga na kumuua mamake Imani

(iii) Viongozi wanatumia mahakama kuendeleza maslahi yao wenyewe. Mf. Nasaba Bora anawafungia raia jela bila makosa. Yusufu anazingiziwa mauaji ya babake ili kumhifadhi Nasaba Bora.

(iv) Hawatilii maanani usalama wa raia. Mf. Imani karibu achomeke katika nyumba iliyoteketea.

(v) Wamejawa na ufisadi. Mf. Nasaba Bora anakula hongo na kujitengenezea faili ili kupata mali. Mwalimu Majisifu anaiba masaa ya kazi. Nasaba Bora anawahonga polisi,makarani wa mahakama na hata majaji.

(vi) Wanakiuka haki za kibinadamu. Mf. Nasaba Bora anamtupa mtoto na kumpagaza Amani mzigo wa kumlea mtoto huyo. Anamtumia Amani kama mtumwa. Anampiga Amani na kumtupa kando ya mto kiberenge.

Mwalimu Majisifu anawabagua watoto wake kwa sababu ya ulemavu.

(vii) Viongozi ni wazinifu Mf. Nasaba Bora anahusiana kimapenzi na Lowela msichana mdogo.

Fao anahusiana kimapenzi na mwanafunzi wake.

(viii)Viongozi wanawatunza wahalifu baada ya kuukomesha uhalifu.mf mwalimu majisifu anapoachishwa kazi kwa kutowajibikia,anapewa kazi nyingine ambapo pia hawajibiki lakini hakuna hatua yoyote.

(ix)Wanaendeleza ukabila na ubaguzi kinasaba.mf Nasaba Bora anapewa cheo cha utemi kwa sababu Mudir wa wilaya ni wa nasaba yake.Mwalimu majisifu anapata kazi kwa sababu anajulikana na wakuu .

(x)Wanatumia mali ya umma kujinufaisha mf.Nasaba Bora anawalazimisha raia kutoa pesa ili kumpeleka mtotoe kusomea Urusi.

(xi)Wanateketeza mali ya umma.mf.Nasaba bora anawatuma askari kuchoma nyumba ya akina Imani. Zozote 10x2=alama20

Q4 T Arege mstahiki meya

(a) Maneno haya yalisemwa na Diwani III
Alikuwa akimwambia Daktari Siki.
Walikuwa nyumbani kwa Diwani III
Diwani III alikuwa anazungumza jinsi Meya amekataa kusikiliza ushauri wake.
Zozote 4 x 1 = 4

(b) Methali mf. Sikio la kufa halisikii dawa. (ala 2)

(c) Mhusika mkuu ni Meya

(I) Meya anaonywa kuhusu <u>ukosefu wa dawa</u>
Anawadaganya kuwa ameagiza dawa

(ii) Meya anashauriwa kuhusu <u>Vifo</u>
Anapuuza anasema huyo mmoja tu.

(iii) Meya anaonywa kuwa baraza halina pesa. Yeye anapuuza na kupeleka watoto wake ng'ambo.

(iv) Meya anajua kwamba kuna <u>mgomo.</u>
Anapuuza mgomo mpaka wageni watarajiwa wanakosa kuwasili.

(v) Sosi anajua hali ya elimu ni duni nchini Cheneo. Anapuuza na kupeleka watoto wake.

(vi) Sosi anajua hali ya <u>matibabu</u>. Afya ni mbaya nchini Cheneo. Yeye anampeleka mke wake ng'ombe baadala ya kuboresha matitabu.

(vii) Meya anaelewa kuwa <u>mazao</u> yamedidimia. Analetewa mayai madogo sana kwa kuwa kuku hawana chakula. Anawalaumu wakulima na hata kusema wasimletee mayai tena.

(viii) Meya anaelewa kuwa baraza halina pesa. Anatoa amri madiwani wasilipe <u>kodi</u> licha ya kushauriwa na mtaalamu wa uchumi.

(ix) Kandarasi. Meya anajua kuwa Bili sio mtaalamu wa mambo ya uchumi lakini anakubali ushauri wake kuhusu kandarasi.

(x) Meya anakubali ushauri wa Diwani kwamba watumie <u>propaganda</u> badala ya kushughulika matatizo ya jamii.

5. Ushauri wa kupotosha
-Meya anashauri waongeze mishahara ya madiwani na askari
-Anunulie madiwani suti za kuvalia wakipokea wageni
- Atumie askari kuzima wafanyakazi wiliogoma.
-Afute wanaogoma ajiri wapya
-Aunde kamati za maendeleo afanye madiwani vinara
- Aandalie vijana mashindano ya nyimbo ambako atawapa zawadi ndogondogo
- Bili alipwe kwa ushauri kwa baraza (wakupotosha)
-Auze fimbo ya meya ng'ambo ajitajirishe
Azingiziye wizi wa fimbo na mgomo wa wafanyakazi.
- atumie dini na muhubiri kuendesha utawala wake
Amfute mwana kandarasi aliyepewa kazi na Meya wa awali
-Adai fidia itakayolipwa mwana kadarasi aliyefurushwa

-Aidhinishe madiwani walipwe nyongeza maramoja nyogeza inayotekelezwa siku mbili tu kabla ya mwezi kuisha
Atenge diwani III katika mikutano wa kujadili maswala ya baraza.
Haja (10 x 2)= alama 20

6(a) Ni maneno ya msimulizi. Anawaza haya baada ya kushindwa kumtoa ushamba mkewe. Ni baada ya kujipa moyo tena wa kutaka kumtoa kinyangaa. Aziza kwa kutaka kujua sababu yake kutovaa viatu nyumbani kwake. Hofu yake sasa ni kuwa hakutaka waliojifunga kuja kumtazama mke wangu namna alivyojirekebisha waondoke na zawadi za vichekesho. (ala.4)

(b)

| Msimulizi | Aziza |
|---|---|
| Ni mbaguzi ambaye aliamini watu wa daraja la chini hawakupaswa kutangamana na watu wa daraja la juu. | Hana ubaguzi na alitangamana na kila mtu |
| Anaathirika na tamaduni za kigeni na kupuuza tamaduni asilia | Ni mwanajadi ambaye hataki kuathiriwa na usasa, Angali anang'ang'ana mambo ya jadi kama vile kutembea bila viatu |
| Anaathirika na elimu na utajiri katika familia na kuzidharau kazi zingine. | Ni mkulima na mfanyikazi. Hili linadhibitika katika mikono yake ambayo imekomaa kutokana na kufanya kazi ngumu |
| Ni msomi na alizaliwa katika familia ya wakwasi | Alitoka familia ya walala hoi na hakupata elimu yoyote |

(Asipolinganisha mwanafunzi amekosea) (alama 8)

(c) Kuchaguliwa mke. Kijana wa kiume katika jamii alioa kutokana na mke aliyechaguliwa na wazazi wake.
- Wana pia walilazimishwa kuoa au kuolewa wakishafika umri wa ndoa.
- Wanawake kudunishwa kama vile kudai kuwa ndio wanaohitaji maongozi ya mume na si kinyume chake.

(al.6)

(d)
- Mbinu zilizotumika
- Tashbihi
- Balagha

(al.2)

## 7. Hadithi fupi

**Damu Nyeusi Na Hadithi Zingine**

Huku ukirejelea hadithi zifuatazao: Samaki Wa Nchi Za Joto, Damu Nyeusi, Mwana Wa Darubini, Kanda La Usufi na Shaka Ya Mambo, fafanua jinsi uozo wa kimaadili uliyoshughulikiwa.

1. **Samaki wa nchi za joto**

(i)Anasa na starehe. Badala ya kusoma Christine akiwa chuo kikuu cha Makerere aliamua kujiingiza katika mapenzi na Peter. Haya si mapenzi ya dhati.

ii)Peter kuwa na <u>Uhusiano wa kimpenzi</u> (ukahaba) na wasichana wengi. Kwa mfano, Daogrecias alisema,nimeona wengi kama nyinyi ambao walipitia katika nyumba hii hapo mwanzoni.

iii) Kuavya mimba.

iv) <u>Malipo duni</u> – wavuvi wanalipwa pesa duni, lakini Peter ni tajiri.
Alinunua samaki kisha kuwauza kwa bei ya juu

v) Biashara haramu – Biashara ya magendo noti bandia. Jagit alikuwa amekuja kumwuzia Peter dola za kimarekani. Hii biashara iliidhinishwa kufanywa tu na Benki kuu ya Uganda.

vi) Kupigwa busu hadharani – vijana walimutusi Christine,"Huyu msichana atakuambukiza ukimwi,ona alivyokondeana.

vii) Matusi – Christine anawatusi vijana wale mabaradhui. Peter naye anatusi Christine.

5-1-5

**2.DAMU NYEUSI**

**(i**)Tukio la Fiona kumdanganya Fikirini eti atamsaidia kumpeleka chuoni,lakini baadaye anamnyanganya bidhaa zake.

**{ii)**Ubaguzi kati ya wazungu na waafrika na Waameerika weusi na Waafrika.kwa mfano Fikirini anashikwa kwa kuvuka barabara huku taa za kuelekeza magari zikiwa zimewaka rangi nyekundu.

-Kuandamwa dukani wakidhani angeiba.

-Chuoni Fikirini ananyimwa alama.

-Maswali ambayo Fikirini anaulizwa-Je kule kwenu watu huvaa nguo?

(iii)Ukware/Usherati-Fiona anamwambia Fikirini kuwa anataka goodtimes.

(iv)Kumvua nguo-Fiona na Bob wanamvua Fikirini huu ni unyama.

Alama 4x1=4

**3.MWANA WA DARUBINI**

**(i)** Kanada kwenda/kupelekwa kufanya kazi akiwa motto mdogo kwa bwana Mwatela

**(ii)** Bwana Mwatela alimchokoza Kananda kwa kumtaka mapenzi na mwisho wake akambaka akawa na mimba.

**(iii)** Kumtishia kuuua iwapo atatoa siri kuhusu motto.

**(iv)** Kumpokonya motto wake

**(v)** Bwana Mwatela alimpa dereva Kananda bure.

**(vi)** Dereva alimuuza Kananda utmwani huko Kongo

**(vii)** Mwakitawa alichochewa dhidi ya mamake ampige kwa fyate.

**(viii)** Ulevi wa Bwana Mwateala ulifanya kumpiga Maria mkewe.

**(ix)** Bwana Mwatela alimdanganya Katana kuwa mamake Mwakitawa amekufa.
(Zozote 4x1=4)

**4.SHAKA YA MAMBO.**

(i) Grace anamdanganya Esther kuhusu uhusiano wao na Kamata.

(ii) Kamata pia anamdanganya Esther kuhusu uhusiano wao na Grace.

(iii) Grace anakataa kumbadilishia Esther zamu ili aingie saa nne mchana mpaka saa nne usiku.

(iv) Grace anamdanganya Esther kumshikia zamu ya mchana kwa sababu alikuwa na mradi muhimu sana Nairobi.

( 4x1=4)

**5.KANDA LA USUFI**

(i) Vijana wanatumia tamasha za muziki vibaya(Masazu)
(ii) Babake Sela anamfukuza Sela na mama yake nyumbani
(iii) Sela kufanya mpango wa kumuiba motto usiku wa halati kwa Rozina
(iv) Wanafunzi k.m. Masazu kutumia tamasha za muziki kutafuta wapenzi(Sela)
(v) Masazu kudai anaumwa na kichwa, ila ni uongo ili apate Sela.
(Zozote4x1=4)

Q8(a) Utanzu wa Fasihi Simulizi unaohusisha matendo pamoja na maneno 2x1=alama 2

(b) Sifa za maigizo
(i) Huigizwa mbele ya hadhira
(ii) Yahitaji uwanja maalum wa kutendea
(iii) Hufungamana na shughuli za kijana k.v tohara
(iv) Sharti pawepo tendo la kuigizwa
(v) Kuna maleba
(vi) Huweza kuambatana na ngoma pamoja na nyimbo.
(vii) Huwa na muundo mahususi

4 x 1 = alama 4

(c)
- ishara za uso nwili na miodoko ambayo inaoana na hali ya kuigiza
- Avalie maleba yanayochukuana na nafasi anayoigiza
- Abadilishe toni na kiimbo kulingana na hali tofauti
- Abadilishe uigizaji wake kulingana na hadhira
- Aitumie lugha kwa ufasaha
- Adhihirishe ukakamavu / ujasiri wakati wa kuigiza

4 x 2 = alama 8

(d)
- huburudisha
- kuhifadhi,kuendeleza utamaduni
- kitambulisho cha jamii
- kukuza umoja
- Nyenzo ya kupitisha maarifa na amali za jamii
- Huakisi mitazamo ya jamii kuhusu masuala mbalimbali
- Husifu tabia nzuri
- Hukuza uzalendo
- kuimarisha ubunifu
- kukuza kipawa cha uongozi
- kuelimisha